**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA**
**SHULE YA SEKONDARI KONGWA**


**NAMBA ZA SIMU:** S.L.P 16
Mkuu wa shule : **0754 396 046** Kongwa
Makamu mkuu wa shule: **0713 007 642** Dodoma
Mwalimu wa malezi : **0684 752 221**


---

**Tarehe ………………**

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI
..........................................................
S.L.P................................................

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KONGWA HALMASHAURI YA WILAYA KONGWA …………**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii .............................. na atasoma tahasusi ya .............

   Shule ya sekondari Kongwa ni shule ya bweni ya wavulana kwa kidato cha tano na sita. Shule hii ipo umbali wa Km 80 kutoka dodoma mjini na Km 16 kutoka barabara kuu Dodoma hadi Dar es Salaam, na KM 1 kutoka stendi ya Kongwa . Ukitokea Dar es salaam utapanda mabasi yanayoelekea Mpwapwa na kushukia Kongwa stendi au ukipanda mabasi yanayoelekea Dodoma utashukia kituo kinachoitwa Mbande.

   Ukitokea Mwanza, Arusha, Iringa, Mbeya, Singida, n.k utapanda mabasi yanayo kwenda Dar es Salaam na kushukia kituo cha Mbande au kama basi linaishia Dodoma mjini utashukia Kituo cha nane nane na kupanda Dala dala au boda boda kuelekea kituo cha mabasi Ndugai. Hapo utakuta daladala zinazoelekea kongwa stendi kwa nauli ya TSH 5,000/=

   Kutoka Mbande kwa wanaotokea Dar es salaam, nauli yake ni **TSH 2000/=** kuelekea Kongwa stendi. Kutoka Kongwa Stendi mpaka shule ilipo utatumia usafiri wa bajaji TSH 3000/= au Boda boda **TSH 1,000/=**

   Muhula wa masomo utaanza tarehe **.....................** na mwanafunzi anatakiwa kuripoti ndani ya wiki mbili za mwanzo, baada ya hapo anaweza kupoteza nafsi ya kujiunga na shule hii.

**Mwanao atapokelewa shuleni akiwa na:**

- Nakala (photocopy) ya cheti cha kuzaliwa na kivuli cha matokeo (result slip)
- Kitambulisho cha Bima ya afya (NHIF, CHF, au aina nyingine ya kitambulisho cha afya)
- Amekamilisha mahitaji yote yapasayo kuja nayo kama maelekezo ya fomu hii
- Fomu ya kupimwa afya iliyojazwa na Mhudumu wa afya na kugongwa muhuri
- Amejaza ahadi/kiapo cha mwanafunzi
- Fomu ya malipo ya benki (bank pay slip) yaliyolipwa katika akaunti ya shule
- Fomu ya utambulisho wa mwanafunzi (fomu hii itajazwa shuleni baada ya mwanafunzi kufika)
- **Bunda la karatasi A4 (ream) mbili (2) nyeupe**

2. MAHITAJI MAALUMU YA KUZINGATIA

**2.1. SARE ZA SHULE**

i. Suruali mbili (kijani jeshi) yenye upana wa inchi 14
ii. Suruali mbili (2) za rangi ya kaki zenye upana wa inch 14 kwa chini
iii. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mirefu
iv. Track suit ya bluu moja (1) ya timu ya taifa ya Tanzania yenye mistari ya njano.
v. Jezi ya rangi nyeusi ya timu ya taifa la Tanzania (Taifa stars) (fulana na bukta yake)
vi. Sweta la kijani jeshi moja (1)
vii. Soksi za kaki jozi mbili (2)
viii. Mkanda mweusi wa ngozi
ix. Viatu vyeusi vya shule ambavyo si vya kufunga na kamba (Visivyo na gidamu)
x. Raba za michezo (viatu vya michezo)

**2.2. VIFAA VYA USAFI**

Kwa tahasusi ya **PCB** waje na vifaa vifuatavyo:

- Kwanja moja (1)
- Squizer moja (1)
- Ndoo lita kumi mbili (2)
- Fagio laini (soft bloom) moja (1)
- Arrows (Dawa ya kusugulia sinki ya choo) lita 2

Kwa tahasusi ya **HGL** wanatakiwa waje na vifaa vifuatavyo:

- Jembe na mpini moja (1)
- Fagio la chelewa moja (1)
- Mopa (1) pamoja na bakuli lake la kukaushia
- Arrow ( Dawa ya kusugulia sinki ya choo) lita 2
- Ndoo ya lita kumi (2)

### 2.3. MAHITAJI YA TAALUMA

Bunda la karatasi nyeupe (Ream A4) mbili kwa mwaka mzima

### 2.4. MICHANGO MBALIMBALI

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

Malipo ya michango mbalimbali iliyopo jedwali **2.4** yalipwe kwenye akaunti ya shule :
**A/C 50301100001 (NMB)- KONGWA SEC. SCHOOL DVT FUND**

### 2.5. MAHITAJI YAKE BINAFSI YA BWENI

i. Godoro lenye ukubwa wa (2 ½ x 6) ft
ii. Mashuka mawili yenye rangi nyekundu
iii. Taulo, vest nyeupe na nguo za ndani za kutosha
iv. Kanda mbili kwa ajili ya kuogea
v. Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
vi. **Chandarua** ya bluu yenye pembe nne
vii. Trunker (sanduku la kuhifadhia vifaa)

NB**:** Kwa wale wanaotokea mbali, unaweza kuvipata vifaa vyote hapa Kongwa kwa bei ya soko.

### 2.6. MAHITAJI YAKE BINAFSI YA DARASANI

I. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ( Mtaala mpya)
II. Madaftari aina ya counter books kumi (10)
III. Disecting kit bag kwa wanafunzi wa mchepuo wa PCB
IV. Laboratory coat kwa wanafunzi wa PCB
V. Kwa tahasusi ya HGL aje na Advanced Learners Dictionary

## 3. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu NA:25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, sayansi na teknolojia yenye dhamana ya Elimu na ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu ya usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini.

Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni, mambo hayo ni pamoja na:

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Sheria na kanuni hizo zinazingatia misingi ya heshima, adabu, uaminifu na tabia njema kwa ujumla.

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia, kauli na vitendo hivyo.

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimia mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri.
2. Hairuhusiwi kwa mwanfunzi kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa mwanafunzi mwenzake
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi:
    a. Kufuga kucha na nywele
    b. Kufuga ndevu
    c. Kunyoa kipara
    d. Kutukana au kutukanana
    e. Kutia dawa nywele na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
    f. Kuvaa vitu kama mapambo mfano; heleni, mikufu ,bangili au vitu vya kiimani rozari,Kofia, kanzu, vilemba na suruali fupi kwani shule hii ni ya serikali.
    g. Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
    h. Kuvaa kaptula na kandambili jikoni na ofisi zote za shule
    i. Kuvaa suruali chini ya kiuno (mlegezo)
    j. Kuvaa nguo za mitindo mfano modo
4. Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma

5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu anapouliza au kujibu swali.

6. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtulivu,asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyosababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa darasani, bwenini, wakati wa kujisomea na katiak mikusanyiko yoyote mfano paredi.

7. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo, mwanafunzi:
    - Aripoti shuleni tarehe ya kufungua na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
    - Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa.
    - Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa.
    - Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki ya uwepo wake shuleni (roll-call), ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya taifa, mikutano ya darasa na n.k.

8. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare za shule kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule.

9. Ni **LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalum na anapaswa kuwa na kibali cha maandishi (pass).
10. Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 2:00 usiku hadi saa 4:30 usiku na kuamka saa 10:00 alfajiri kwa ajili ya prep. ya asubuhi (morning prep.).
11. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia umeme kwa shughuli yoyote ile awapo bwenini au darasani.

12. **USAFI:** mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
13. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha mkuu wa shule, na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa mkuu wa shule.
14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule ya sekondari Kongwa muda wote akiwa ndani na nje ya mipaka ya shule, achomekee shati lake. **Mavazi yasiyo ya shule hayaruhusiwi kabisa.**

**15.** Hairuhusiwi kujihusha na mikutano ya kisiasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

**16. HAIRUHUSIWI KWA MWANAFUNZI KUMILIKI NA KUTUMIA SIMU AWAPO SHULENI AU NJE YA MIPAKA YA SHULE.** Mawasiliano yoyote ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yapitie kwa mwalimu mlezi (patron)

**MAENEO YASIYORUHUSIWA**

Mwanaafunzi harususiwi kufika/ kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:

- Ofisi za shule
- Bohari za shule
- Kwenye disko, ngoma, muziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ya shule
- Maabara
- Baa, kilabuni, vibanda vya PS, mabanda ya kuonyeshea video au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine.
- Nyumba za wageni (guest house).
- Nyumba za walimu/watumishi.

**ZINGATIA:**

Unataarifiwa kuwa shule hii ni ya serikali wala siyo ya dini fulani, aidha inazingatia katiba ya nchi ya Tanzania, uhuru wa kuabudu, hivyo, wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao, pia kumepangwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya Alhamisi na kila siku jioni baada ya chakula cha jioni.

Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba zao za kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. Tofauti na hayo, mzazi/,mlezi anaruhusiwa kumtafutia mwanafunzi shule ya dini endapo mwanafunzi huyo ana wito wa dini husika.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga, ulawiti na ubakaji
3. Ulevi wa aina yoyote kama utumiaji wa madawa ya kulevya, pombe, sigara, bangi, mirungi n.k
4. Makosa ya jinai
5. Kuoa
6. Kuharibu kwa makusudi mali za uma
7. Kupigana au kumpiga mwingine
8. Kudharau bendera ya taifa
9. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya mkuu wa shule
10. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma kwa namna yoyote
11. Kutoa lugha ya matusi
12. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
13. Kutohudhuria vipindi vya darasani, dini au prep.
14. Mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama vile laini au chaja
15. Kumiliki vifaa mbalimbali kama vile redio, pasi n.k
16. Kupata wastani wa alama chini ya 60% katika masomo yake.
17. Kukosa kufanya mitihani na majaribio kwa makusudi

**KARIBU SANA KONGWA SEKONDARI**

**..................................**
**ALEX A. SALUM**
**MKUU WA SHULE (0754 396 046)**

**AHADI /KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi .................................................... kidato cha tano mchepuo ................. ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Kongwa, kidato cha tano mwaka 2025/2026 ninaipokea na kuikubali nafasi niliyopewa na serikali kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya taifa na shule ya sekondari Kongwa.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ni ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Ninaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufikisha makusudio haya, ni hujuma kwa taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo, ninaahidi kuwa nikiwa hapa shuleni yafuatayo nitayazingatia:

- Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu
- Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyosoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
- Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapa shuleni
- Nitafaulu katika mitihani yangu yote na kamwe sitapata chini ya alama za ufaulu wa shule ambazo ni 60%

Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi wangu................................. (jina la mzazi) kwa ajili ya hatua zaidi.
Saini ya mwanafunzi.......................... tarehe ......................

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ...................................................... ninakubali mtoto wangu ........................................ kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Kongwa mwaka 2025/2026. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa, ikiwa ni pamoja na kufanya vizuri katika masomo

**Anwani yangu ya kudumu ni .......................... namba ya simu ..........................**

**Saini ya mzazi/mlezi .............................................. tarehe ....................................**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ANDIKA KWA HERUFI KUBWA)**

JINA KAMILI ........................................................................................ (MAJINA MATATU)

SHULE YA SEKONDARI ULIYOTOKA........................................................................

WILAYA ........................................................... MKOA...........................................................

ANWANI YA ULIKOTOKA..........................................................................................

TAREHE YAKUZALIWA..............................................................................................

JINA KAMILI LA BABA ...................................NAMBA YA SIMU................

JINA KAMILI LA MAMA ...................................NAMBA YA SIMU................

UHUSIANO WAKO NA MLEZI.......................................

**TAJA NDUGU WATATU WA KARIBU WATAKAOFIKA SHULENI PINDI JAMBO LOLOTE LIKITOKEA LINALOMHITAJI MZAZI AU MLEZI IKIWA HAWAPO**

1. ..........................................................................
   S.L.P...............................................................
   NAMBA YA SIMU .....................................
   UHUSIANO .................................................

2. ..........................................................................
   S.L.P...............................................................
   NAMBA YA SIMU .....................................
   UHUSIANO .................................................

3. ......................................................................
   S.L.P...............................................................
   NAMBA YA SIMU .....................................
   UHUSIANO ............................................

**MEDICAL EXAMINATION FORM (FOMU YADAKTARI)**
**FROM THE HEAD MASTER, KONGWA SECONDARYSCHOOL**

TO THE MEDICAL OFFICER,
.....................................................
NAME OF STUDENT : ............................................
AGE: ...........................................................................

| MEDICALHISTORY | YES | NO |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Pepticulcers | | |
| Epilepsies | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidneyproblem | | |
| Anemia | | |
| Neurosis | | |

Physical Examination

1. Respiratory system
2. Cardio vascular system
3. Urinary system
4. Reproductive system
5. Eye
6. E.N.

Investigate

1. Blood-HB................................................
   WBC............................................
   ERS.............................................
   VDRL Test ............................
2. Urine - Sed....................................
   Stool....................................

I have examined and consider that he is physical and mental fit/unfit for further education
Signature ....................................................... Date ...................

***KITAMBAA CHA KIJANI JESHI***




CS CamScanner

Authorize the system to edit this file.

Authorize

Edit Annotate Fill & Sign Convert All